
Congolese Swahili

# mwili wako chaguo lako



**Unyanyasaji kuhusu sehemu za ziri ni kosa.**

**Kamwe si sawa kwa mtu kutumia nguvu au vitisho ili kukufanya ufanye jambo lolote linalokufanya ukose raha**

**Ikiwa wewe au mtu unayemjua amekumbwa na unyanyasaji  wa kijinsia, unaweza kupata usaidizi kwa**

**Polisi ya Queensland:** Ita 000 (zero mara tatu)

**National Sexual Assault Service:**
(Huduma ya Kitaifa ya Unyanyasaji wa kijinsia
Ita 1800 737 732
(simu ya bure, masaa 24, siku 7 kwa wiki)

**Watafsiri wa bure:** Pigia Translating and Interpreting Service (TIS) (Huduma ya Utafsiri na Ukalimani (TIS)) kwa 131 450.
Mtafsiri ataongeya  na huduma yoyote unaitaji kwa Bure

**1** Jua haki zako

**2** Zungumza na mtu unayemuamini

**3** Pata msaada

1

## Jua haki zako

**Una haki ya kuchagua nani wa kuwa naye ngono ya karibu.**


**Ngono na kukaribiana kimapenzi vinaweza kujumuisha kuguswa kingono, kulalana, picha za ngono na kutuma ujumbe wa ngono.**

**Kukulazimisha kushiriki katika mojawapo ya shughuli hizi ikiwa haujakubali kwa kupenda  kwako  ni kinyu me ya sheria.**

**Katika  Australia, mtu hawezi kukugusa, kukutishia, kupeana picha za ngon o zisizotakiwa zako  au pamoja naweye, au  kutoa maoni kuhusu ngono kwako au kukuhusu weye bila ruhusu.**

**Makosa ya kingono ni uhalifu mkubwa na wahalifu wanaweza kufungwa gereza miaka 14**

**Kuripoti uhalifu au kuwa mwenye kutendewa uhalifu haitakuwa na matokeo ku visa yako au hali ya kazi.**



## Je, Unyanyasaji wa kijinsia ni nini?

Unyanyasaji  wa kijinsia unaelezea a ina mbalimbal i za uhalifu wa kingono, ikiwa ni pamoja na:

- **UBAKAJI**, ambapo ni pale unapolazimishwa kufan ya ngono(uke, mkundu au mdomo).
- **KUGUSWA KUSIKOTAKIWA** kwa aina yoyote chini au juu ya nguo yako.
- **KUVUA CAPOTTE** mbele au wakati wa ngono bila ruhusa yako yako.
- **NGONO YA KULAZIMISHWA**, ambayo ni wakati mtu anakutiya mukazo au kukuchenga ili ufanye mambo ya ngono ambayo hutaki kuyafanya.
- **USUMBUFU WA KUFUATILIA MTU BILA YEYE KUTAKA**, ambayo ni wakati mtu anakufuata au kukufuatilia.
- **KUKUANGALIA BILA RUHUSA YAKO** wakati unafanya mambo ya siri au uko buchi.
- **KUWEKA WAZI BILA ADABU**, ambayo ni wakati mtu anakuonyesha sehemu za siri za mwili wake.
- **KULAZIMISHWA KUTAZAMA AU KUSHIRIKI KWENYE PICHA ZA NGONO**, ikiwa ni pamoja na mtu kukupiga picha bila ruhusa yako, kukulazimisha kuonekana kwenye video au kukufanya utazame film ya ngono.
- **MESSAGE ZA NGONO**, ambayo ni kushirikisha picha zako za uchi bila ruhusa yako au kukutumia picha za uchi ambazo hutaki.

# Idhini ya kingono ni nini?

## KUTOLEWA KWA BURE

Kukubali ni wakati unapochagua bila mukazo, kudanganywa au ushawishi wa dawa za kulevya au pombe.

## SHAUKU

Wakati linapokuja ulizo la ngono, unapashwa kukubali tu kufanya mambo UNAYOTAKA kufanya, si mambo ambayo unahisi unatarajiwa kufanya.

## MAALUM

Kukubaliana na jambo moja (kama kwenda katika chumba c ha kulala) haimaanishi  kuwa umekubali kufanya jambo lingine (kama kufanya ngono).
Ikiwa mtu anakubali kuvaa kond omu na kisha hakubali, hii sio ku itika.

## KUBADILI MAWAZO

Unaweza kubadilisha mawazo yako wakati wowote wakati wa ngono, hata kama umefanya hivyo hapo mbele na hata kama nyote wawili mko uchi kitandani.

## KUFUNGWA NA MDA

Kutoa kibali kwa wakati fulani haimaanishi kuwa umetoa kibali kwa jambo lile lile wakati mwingine wowote.

## KIMYA SI KUITIKA

Watu wengi hupatwa na dalili za kimwili kama kutoa jasho au kutetemeka wakati wanaogopa sana.
Kwa sababu tu haukusema kitu, haimaanishi kuwa umeitika.

## 2 Zungumza na mtu unayemwamini

Kuzungumza na rafiki unayemwamini, mwanafamilia au huduma ya ushauri inaweza kukusaidia kuamua cha kufanya nyuma. Hata kama utaamua kutoripoti hiyo unyanyasaji wa ngono, kuna maeneo mengi ambapo unaweza kupata usaidizi na msaada wa siri bila malipo.

**1800RESPECT**
Hutoa ushauri wa simu na mtandaoni kwa watu walio pata shida ya unyanyasaji wa ngono na unyanyasaji wa nyumbani.
1800 737 732
www.1800respect.org.au

**Queensland Sexual Assault Helpline (Namba ya Msaada ya Unyanyasaji wa Ngono ya Queensland)**
Usaidizi wa simu na ushauri kwa mtu yeyote ambaye amenyanyaswa kingono au kunyanyaswa na mtu yeyote anayehusika na mtu anayemjali anaweza kuwa alishambuliwa au kunyanyaswa.
1800 010 120
www.dvconnect.org
7:30am-11.30pm siku 7

**Lesbian Gay Transgender Bisexual Intersex and Queer (LGBTIQ) (Msagaji Mashoga Aliyebadilisha jinsia Mbili na Mwenye Jinsia Mbili (LGBTIQ)) Maalumu:**
**QLife**
Hutoa usaidizi wa simu na wavuti kwa watu wa umri wa myaka yote.
Piga: 1800 184 527
3pm mpaka saa sita za usiku.
Siku 7 kwa wiki.
Usaidizi na msaada unapatikana ikiwa umehangaishwa kingono au kunyanyaswa.

3

# Pata msaada

**Kuna huduma tofauti ambazo zinaweza Kuna huduma mbalimbali ambazo zinaweza kukupa usaidizi. Mtu yeyote, ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa kimataifa na wageni wanaweza kupokea usaidizi na msaaa kutoka kwenye huduma hizi.**

## Msaada wa matunzo

Ikiwa umenyanyaswa kingono, unaweza kupata huduma ya matunzo bila malipo katika idara ya dharura (dépatement ya urgence) ya hopital yoyote ya leta.

Huduma za Unyanyasaji wa Ngono wa Afya ya Queensland zinapatikana bila malipo (huhitaji kadi ya Medicare) saa 24 kwa siku).

Huduma hizi hutoa habari, ushauri, matunzo na uchunguzi bila malipo kwa yeyote ambaye amenyanyaswa kingono.

Wanaweza kutoa upimaji wa magonjwa inayoambukia kupitia sehemu za siri na kuzuia mimba.

Ushahidi wa kimatunzo unaweza kusaidia kuonyesha kilichotokea.

Uchunguzi wa unyanyasaji wangono bora kufanywa katika masaa 24 ya kwanza.

Uchunguzi unaofanywa mpaka siku saba nyumba ya shambulio unaweza kutoa ushahidi wa lazima ambao unaweza kutumika katika tribunal, ikiwa shida hiyo itapelekwa mbele zaidi.

**ONGEYA NA GP WAKO AU 13HEALTH (13 43 25 84) KWA HABARI NA HUDUMA ZA KWENYE UNAISHI.**

---

**Hii ni marekebisho ya rasilimali (resources) iliyotolewa na City of Sydney, Redfern Legal Centre and StudyNSW (Jiji la Sydney, Kituo cha Sheria cha Redfern na StudyNSW).**

## Msaada wa kisheria

Huduma za kisheria za bure zinaweza kukupa ushauri wa siri kuhusu chaguo zako. Ushauri huu unaweza kuhusiana na kwenye unaishi, elimu na kwenye unatumika pamoja na kutoa ripoti kwa polisi. Zifuatazo ni bure, huduma za kisheria za kitaalam (services légaux za ba spécialistes).

**Women's Legal Service (Huduma ya Kisheria ya Wanawake)**
Community legal centre (kituo cha sheria cha jamii) hutoa ushauri na taarifa za kisheria bila malipo kwa wanawake.
1800 957 957 | https://wlsq.org.au

**Legal Aid (Msaada wa Kisheria)**
Hutoa habari za kisheria, ushauri na kusimamiyana.
1300 651 188 | www.legalaid.qld.gov.au

**ILI KUPATA MSAADA KUTOKA KWA HUDUMA ZA WENYE WALIPATWA NA SHIDA**

Ikiwa wewe ni mtu mwenye alipatwa na uhalifu, unaweza kuwa na haki ya kupata huduma mbalimbali za bure ikiwa ni pamoja na ushauri, usaidizi wa kifedha na usaidizi wa kisheria.

**Victim Assist Queensland (Msaada wa Mwathirika Queensland)**
1300 546 587 (9am-5pm)

## Kutoa ripoti kwa polisi

Unyanyasaji kuhusu sehemu za ziri ni kosa. Kuwa mwathirika wa uhalifu hakutaathiri viza yako au hali ya ajira. Polisi katika Australia watachunguza ripoti yako na kuifuatilia ili kuhakikisha usalama wako na usalama wa wengine. Unaweza kutoa ripoti kwa polisi kwa:

- kupiga simu sifuri tatu (000)
- kuhuzuria kituo cha polisi ukijifikia
- kuripoti tukio hilo bila kujulikana kupitia Crime Stoppers (Wazuia Uhalifu) kwa namba1800 333 000.

Huduma za usaidizi zinaweza pia kukusaidia kutoa ripoti kwa polisi.

CITY OF SYDNEY | Redfern Legal Centre | NSW GOVERNMENT | true relationships & reproductive health